



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

Barua zote ziandikwe na kutumwa kwa:

Simu: +255 262 965 732(Direct line)

Nukushi: +255 262 965 732

Barua Pepe: ded@sikongedc.go.tz

Tovuti: www.sikongedc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge

4 MTAA WA BOMANI

S.L.P. 70,

45382 SIKONGE - TABORA

Unapojibu tafadhali taja:

27/04/2023

Kumb.Na.HWS/M.10/15/VOL.II/39

MABADILIKO YA TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge alitangaza nafasi za kazi za watendaji wa vijiji daraja la III kupitia tangazo lenye Kumb. Na.HWS/M.15/VOL.II/37 la tarehe 19 Aprili, 2023 baada ya kupokea kibali cha ajira mpya kwa mwaka 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge amepokea maelekezo kutoka kwa Katibu wa Sekretarieti ya ajira katika Utumishi wa Umma kuwa, kwa mujibu wa kanuni Na. 22(1, 2) ya kanuni za uendeshaji wa shughuli za Sekretarieti ya ajira kama ilivyorekebishwa kupitia gazeti la Serikali Na. 580 la 2022 kuwa inaelekeza kutumika kwa kanzi data ya waliofaulu usaili na kupangiwa vituo vya kazi pale inapotokea fursa ya ajira.

Kwa kuwa Halmashauri ya wilaya ya Sikonge ilitangaza nafasi **05** za Mtendaji wa Kijiji daraja la III Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kufanya usaili ambapo wasailiwa wengi walifaulu na kwa kuwa nafasi zilikuwa chache hawakupangiwa vituo vya kazi. Hivyo, wasailiwa hao walifaulu na kukosa fursa ya kuajiriwa wataitwa kujaza nafasi **05** zilizotangazwa. Kwa maelezo haya **ninasitisha** maombi ya nafasi za ajira ya Watendaji wa Vijiji daraja la III zilizotangazwa kwa tarehe tajwa hapo juu.

Naomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

Nico A. Kayange

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)

SIKONGE

**MKURUGENZI MTENDAJI
WILAYA - SIKONGE**